


# MIKAKATI YA KUELEKEA KUFUNGUA TENA

## Orodhahakiki ya mpango wa kufungua tena shule

## Usimamizi wa Biashara na Fedha

OPPORTUNITY EduFinance

# JINSI YA KUITUMIA MIKAKATI YA KUELEKEA KUFUNGUA TENA.

## UTANGULIZI:

Kufungwa kwa shule kumekuwa na madhara makubwa katika shule duniani kote. Sisi, kwenye mradi wa Opportunity EduFinance, kwa msaada wa timu yetu ya Wataalamu wa Elimu, tumeandaa mwongozo huu ili kuwasaidia viongozi wa shule kama vile wewe mwenyewe wakati unaandaa mipango ya kufungua tena shule yako pindi masharti yatakapolegezwa.

Tunatumaini kuwa hii itakuwa njia nzuri kwako kupanga na kuona jinsi ulivyo tayari kufungua tena shule yako.

## KINACHOJUMUISHWA KWENYE MWONGOZO:

Kila mwongozo unashughulikia moja ya maeneo matano ambayo yatahitaji uzingatiaji na mabadiliko kadri unavyotarajia kufungua tena shule yako. Maeneo haya ni:

- Usimamizi wa Biashara na Fedha
- Ushirikishwaji wa Wazazi
- Mazingira Safi na Salama Yanayofaa kwa Mafunzo
- Ushirikishaji wa Wafanyakazi
- Ufundishaji na Ujifunzaji

Maeneo matano yamegawanywa katika vipindi vitatu kutegemea wakati ambapo kiongozi wa shule atakapokuwa anapafikiria kupachukulia hatua. Vipindi vya wakati ni:

- Kabla ya Kufungua Tena
- Wakati wa Kufungua Tena
- Baada ya Kufungua Tena

Kwa kila kipindi cha muda na kwa kila eneo, mwongozo unapendekeza hatua ambazo kiongozi wa shule anapaswa kuzichukua wakati shule zimefungwa na wakati zinafunguliwa tena.

Kila hatua inayopendekezwa katika muda wa vipindi viwili vya kwanza ‘Kabla ya Kufungua Tena’ na ‘Wakati wa Kufungua tena’ vimeelezwa kwa kina zaidi chini ya ‘Vifaa vya Kusaidia’ kukuwezesha kupanga ipasavyo kwa ajili ya utekelezaji wa hatua hizi. Kundi la mwisho ‘Baada ya Shule Kufunguliwa Tena’ linatoa mawazo kuhusu ni hatua gani zinazofuata ambazo shule inaweza kuchukua baada ya kufungua tena.

## ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE:

Wakati utakapomaliza kuchunguza maudhui tunakushauri kuikamilisha Orodhahakiki ya Mpango wa Kufungua Tena Shule. Orodhahakiki inakuhitaji kufikiria ni nani atawajibika kufanya vitendo fulani – huyu anaweza kuwa mmiliki, mwalimu mkuu, walimu waliotajwa, viongozi wa wafanyakazi,

mameneja wa maeneo, watawala wa shule na wanajamii wa kujitolea. Sehemu ya pili inauliza 'Itafanyika lini' hapa unaweza kupanga kipindi cha muda kwa ajili ya shughuli zilizopangwa – tarehe iliyopangwa au siku za kurudia kama vile kila Jumatatu.

# USIMAMIZI WA BIASHARA NA FEDHA.

<table>
<tr><th></th><th>Kabla ya Kufungua Tena</th><th>Wakati wa Kufungua Tena</th><th>Baada ya Kufungua Tena</th></tr>
<tr><td rowspan="3">Akiba ya Fedha za Shule</td><td colspan="2">Bainisha njia mbadala za kuongeza mapato tofauti na ada za shule.</td><td rowspan="3"></td></tr>
<tr><td colspan="2">Bainisha njia ambazo unaweza kupunguza gharama za shule ili kuhakikisha kutokwama kwa uendeshaji wa shule.</td></tr>
<tr><td>Tathmini kiwango cha matumizi yako ya fedha za shule ili kuelewa kama uendeshaji wa shule utamudu kwa kipindi gani kwa akiba ya fedha iliyopo.</td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="2">Ada za Shule</td><td>Hakikisha uwiano wa ada inayokusanywa.</td><td>Waunganishe wazazi na taasisi za ndani za fedha kama wateja wa mikopo ya ada ya shule ili kuhakikisha kuna ukusanyaji mkubwa wa ada.</td><td rowspan="2">Endeleza mawasiliano ya kawaida na wazazi kuhusu malipo ya ada za shule kwa wakati.</td></tr>
<tr><td>Anzisha njia za kukusanya ada za shule wakati ukiendelea na uepukaji wa msongamano mf. kukusanyaa fedha kwa njia ya simu za mikononi.</td><td>Anzisha njia rahisi za malipo ya awamu kwa wazazi ambao wamepoteza kazi/vyanzo vyao vya mapato kutokana na ugonjwa wa korona.</td></tr>
<tr><td>Fedha za Shule</td><td>Hakikisha au pata fedha za kutosha/mtaji wa kazi ili kutekeleza hatua za usafi katika shule.</td><td></td><td>Anzisha kikundi cha akiba na uwekezaji kwa wafanyakazi ambacho kitasaidiwa na kiongozi wa shule.</td></tr>
</table>

# KABLA YA KUFUNGUA TENA.

## BAINISHA NJIA MBADALA ZA KUONGEZA MAPATO TOFAUTI NA ADA ZA SHULE.

### Muktadha

Mapato muhimu zaidi kwa shule ni yale yanayotokana na ada za shule. Hata hivyo, wakati shule zilipofungwa, uwezo wa wazazi kulipa ada za shule uliathiriwa, ambapo hali hiyo imeathiri ukusanyaji wa ada na mapato ya shule.

Kwa walimu, mshahara kutokana na kufundisha ni chanzo pekee cha mapato. Lakini kutokana na ukosefu wa ada za shule zilizokusanywa, uwezo wa shule wa kulipa mshahara pia umeathiriwa.

Licha ya changamoto zinazoonekana, wakurugenzi wa shule wanaweza wakajiingiza katika shughuli zingine ambazo zinaweza kuongeza mapato kwa shule.

### Kutekeleza katika Shule Yako

Kabla ya kutekeleza shughuli yoyote, viongozi wa shule wanapaswa kuamua ni kazi gani zinazofaa kwao katika muktadha wao. Shughuli zifuatazo zinaweza kuwawezesha viongozi wa shule kuongeza mapato yao:

- Ukulima unaweza kuzalisha mapato kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya shule. Ardhi ya shule inaweza kutumiwa kwa ajili ya shughuli za ukulima ikiwa ni pamoja na upandaji wa mazao na mboga za majani. Pia ufugaji wa wanyama unaweza kuanzishwa ili kuongeza katika uzalishaji wa mazao na mboga za majani. Uzalishaji huu unaweza kutumiwa kusaidia programu ya utoaji wa chakula shuleni.
- Kutoa huduma za uegeshaji wa magari ndani ya mazingira ya shule kwa tozo.
- Kukodisha mali na mabasi ya shule wakati wa likizo. Wakati huu, shule zinaweza kukodisha mali zake na mabasi yake ili kuzalisha mapato ya ziada kwa ajili ya shule.
- Kuanzisha mradi wa madaftari ya masomo katika ngazi ya shule ili kuyauza kwa wazazi. Mradi wa madaftari ya masomo unaweza kufanywa kila mwezi, na wazazi kuyarudisha shuleni mwishoni mwa wiki au mwezi kwa ajili ya kusahihishwa. Yawe na mazoezi kulingana na ngazi za wanafunzi.
- Kuzungumza na benki iliyo karibu yako ili kusaidia mkopo wa mtaji wa kazi ili kuwezesha kifedha uendeshaji wa shule wakati unaanza kupanga mchakato wa kufungua tena.

## TATHMINI KIWANGO CHA MATUMIZI YAKO ILI KUELEWA NI KWA MUDA GANI SHUGHULI ZA SHULE ZINAWEZA KUENDELEA KWA AKIBA YA FEDHA ILIYOPO SASA.

### Muktadha

Ukokotoaji wa kiwango cha matumizi ya fedha ya shule yako utakusaidia kufanya uamuzi wa kimkakati kuhusu ni kwa muda gani unaweza kumudu gharama wakati shule yako ikiwa imefungwa. Hili nila muhimu pia ili kuamua iwapo unaweza kuendelea kuwalipa wafanyakazi na ni kwa muda gani.

### Kutekeleza katika Shule Yako

Hatua zifuatazo zinahitaji kuchukuliwa katika kukokotoa kiwango cha matumizi ya fedha za shule

1) Viongozi wa shule wanapaswa kukokotoa akiba ya fedha kwanza. Hii inajumuisha fedha zilizo mkononi, akaunti ya benki ya shule na bakaa katika akaunti za akiba za shule.
2) Kukokotoa fedha za mapato ya kila mwezi zilizotarajiwa wakati shule zimefungwa: Mapato halisi yaliyotarajiwa yatokane na ada za shule.
3) Kukokotoa gharama za kila mwezi wakati shule zimefungwa: Mapato halisi ikiwa ni pamoja na mishahara na bili za maji na umeme ambazo ungepaswa kulipa wakati shule zimefungwa (tafadhali angalia pendekezo linalofuata kwa ajili ya orodha yenye maelezo ya gharama)
4) Kukokotoa kiwango cha matumizi ya fedha: Hiki hukokotolewa kwa kutoa gharama zako za mwezi kutoka katika mapato yanayotarajiwa ya mwezi. Kiwango cha matumizi ya fedha kitakuwa hasi iwapo mapato yanayotarajiwa kwa mwezi ni sifuri
5) Kukokotoa fedha za kulipia madeni: Fedha za kulipia madeni zinakokotolewa kama Akiba ya Jumla ya Fedha (imekokotolewa katika hatua ya 1)/ Kiwango cha matumizi ya fedha (kimekokotolewa katika hatua ya 4). Jambo hili huzisaidia shule kuamua ni kwa miezi mingapi zinaweza kujiendesha kabla hazijaishiwa na fedha.
6) Katika mfano wa hapa chini, fedha za kulipia madeni iwapo shule itaendelea kulipa Mishahara kwa 100% ni 725/600 = mwezi 1.2 au siku 36.

| **Akiba za Fedha** | | | |
|---|---|---|---|
| Fedha Zilizopo | 75 | | |
| Akaunti ya Shule | 150 | | |
| Akaunti za Akiba ya Shule | 500 | | |
| **Jumla ya Akiba ya Fedha** | **725** | | |
| **KIWANGO CHA FEDHA ZILIZOTUMIKA** | Kwa Mwezi- Shule ikiwa imefunguliwa | Kwa Mwezi- Shule ikiwa imefungwa (Mshahara 100%) | Kwa Mwezi- Shule ikiwa imefungwa (Mshahara 80%) |
| **Fedha Zinazoingia** | | | |
| Ada za Shule zinazotarajiwa kupokewa | 1500 | 100 | 100 |
| Mauzo ya Bustani ya Shule yametoa | 50 | 200 | 200 |
| **Jumla ya Fedha zote Zilizoingia** | **1550** | **300** | **300** |
| **Fedha Zinazotoka** | | | |
| Mishahara ya Walimu | 600 | 600 | 480 |
| Mishahara ya Wafanyakazi Viongozi | 300 | 300 | 240 |
| Huduma | 50 | 0 | 0 |
| Mafuta ya basi la shule | 35 | 0 | 0 |
| Maduka ya vinywaji | 45 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Fedha zote Zilizotoka** | **1030** | **900** | **720** |
| **Mapato Yaliyozalishwa (au Kiwango cha Matumizi ya Fedha kama ni hasi)** | **520** | **(600)** | **(420)** |

Ni kwa namna gani ukokotoaji wa kiwango cha matumizi ya fedha huzisaidia shule katika hali ambapo akiba za fedha na fedha zinazoingia hupungua mpaka sifuri kutokanana kufungwa kwa shule?

Kufungwa kwa shughuli za kiuchumi nchi nzima, kumezitumbukiza biashara nyingi katika hasara, ikiwa ni pamoja na shule. Shule nyingi zimetumia akiba zao zote za fedha, hazijakusanya mapato yoyote kwa namna ya ada za shule tangu shule zilipofungwa mwezi Machi.

Shule zinawezaje kuinua mapato na kiwango cha matumizi ya fedha za shule kitaonekana wapi katika mpango wa shule katika hali hiyo?

- Angalia njia mbadala za kuongeza mapato: Katika sehemu iliyopita, tumebainisha kwa kina njia nyingi za kuongeza mapato. Shule zinapaswa kufikiria kuhusu shughuli hizi (ikiwa ni pamoja na ukulima, ukodishaji wa mali za shule n.k.) pale ambapo inawezekana ili kuongeza haraka fedha zinazohitajika kwa ajili ya kujipanga shule zitakapofunguliwa tena.
- Kuacha Kutumia Mali: Shule zifikirie kuacha kutumia au kuuza mali katika kipindi kifupi. Kwa mfano, kutokana na utaratibu wa kuepuka msongamano uliopo, shule nyingi zitahitajika kuacha kwa muda matumizi ya mabasi ya shule. Katika mazingira hayo, wakuu wa shule wanaweza kufikiria kuacha kutumia mali hizi ili kuongeza akiba zao za fedha. Mali nyingine yoyote ambayo haitumiki inaweza kuachwa kutumiwa ili kukidhi mtaji wa kazi unaohitajiwa na shule
- Mikopo ya mtaji wa kazi: Benki mahalia zitapaswa kuongeza tena mikopo kwa shule ili kukidhi mahitaji ya haraka ya mtaji wa kazi. Viongozi wa shule wawasiliane na benki zao mahalia ili waombe mikopo ya mitaji ya kazi. Pia shule zinaweza kwenda kwenye vyombo vya serikali za mtaa au wizara za elimu kuona kama zinaweza kupata mikopo ya haraka ya muda mfupi au ruzuku ili kukidhi mahitaji ya mtaji wa kazi wa shule.
- Kuwafikia wazazi: Kudumisha mawasiliano na wazazi ni muhimu ili kuhakikisha kwamba wanawarudisha watoto wao shuleni mara shule zitakapofunguliwa tena. Wakuu wa shule wasisite kuwafikia wazazi ambao wanajua wanaweza kuwalipia watoto wao ada zilizobaki za shule.

Mara tu shule zinapomudu kujipatia kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya kuongeza akiba ya fedha zao, shule hizo zitapaswa kutathmini kiwango chao cha matumizi ili kuweka vipaumbele vya matumizi na kuhakikisha kwamba akiba hizi za fedha zinakuwapo hadi shule zitakapopokea malipo ya ada yaliyobaki kutoka kwa wazazi. Vilevile, ili kudumisha mtiririko wa kawaida wa mapato, shule zinapaswa kubuni njia mbalimbali zinazoweza kuongeza mapato kwa mtazamo wa muda mrefu.

## ANGALIA NJIA AMBAZO UNAWEZA KUPUNGUZA GHARAMA ZA SHULE ILI KUHAKIKISHA UENDESHAJI MZURI WAKATI WA KIPINDI CHA KUFUNGWA KWA SHULE

### Muktadha

Kuna uwezekano kwamba shule zinatakiwa kuendelea kufungwa kwa kipindi kirefu. Hili linazihitaji shule kuendelea kufundisha na kujifunza kwa masafa na pia kuwalipa walimu wao kwa kadri inavyowezekana. Hili linafanya iwe muhimu sana kwa shule kutafuta njia za kupunguza gharama ili kuhakikisha kwamba shule zinaweza kuendelea wakati wa zuio la kutotoka nyumbani na kufunguliwa pale zuio la kutotoka nyumbani litakapoondolewa.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Lengo linapaswa kuwa ni kuweka akiba ya fedha nyingi kwa kadri iwezekanavyo. Hili linaweza kuzihitaji shule kuandaa orodha na kukokotoa gharama zake zote za kila mwezi. Gharama za kila mwezi zinajumuisha:

- Mishahara ya wafanyakazi
- Bili za huduma ikiwa ni pamoja na umeme, maji na kodi za pango
- Gharama za Basi la Shule

- Chakula
- Vifaa vya shule
- Ada za Udhibiti
- Marejesho ya Mkopo

Baada ya kubainisha gharama za kila mwezi, shule zibainishe gharama ambazo si za lazima na kujaribu kuziondoa wakati wa kipindi cha kufungwa kwa shule. Baadhi ya mifano inajumuisha:

- Kuchunguza mikataba ya ajira na kutafuta njia za kupunguza mishahara. Hii inaweza kujumuisha kuwataka walimu kuchukua mishahara pungufu wakati wa kipindi cha kufungwa kwa shule au kuwabadili baadhi ya walimu kuwa walimu wa muda.
- Iwapo baadhi ya majukumu ni rahisi kubadilishwa au hayahitajiki, fikiria kuzipunguza nafasi hizi kwa kipindi cha kufungwa kwa shule. Kwa mfano, wafanyakazi wa utawala
- Kuzungumza na benki yako kuhusu kuacha kwa muda kurejesha marejesho wakati shule zinapokuwa bado zimefungwa
- Kuzungumza na mpangishaji wako kuhusu uwezekano wa kupunguza kodi ya pango au kuacha kwa muda kulipa kodi hiyo wakati shule zinapokuwa bado zimefungwa

## ANZISHA NJIA ZA KUKUSANYA ADA ZA SHULE WAKATI UKIENDELEA KUEPUKA MSONGAMANO MF. KWA NJIA YA SIMU ZA MIKONONI

### Muktadha

Wakati shule zimefungwa itakuwa muhimu kuendeleza mawasiliano ya kawaida na wazazi kuhusiana na muda wa malipo ya ada za shule. Kwa vile matembezi ya kukutana ana kwa ana yamekatazwa, viongozi wa shule wanapaswa kubainisha njia ambazo wanaweza kuwafikia wazazi na kukusanya ada kielektroni.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Tafiti njia mbalimbali kwa ajili ya kukusanya ada za shule kwa masafa na kuamua njia ipi itakuwa bora kwa shule yako. Hapa kuna njia za kukusanyia ada za shule wakati ukiendelea kuepuka msongamano:

- Ujumbe mfupi wa benki unaojumuisha misimbo mifupi na fedha kwa simu za mikononi – Akaunti ya shule iliyosajiliwa ya huduma za fedha kwa simu za mikononi au misimbo mifupi inayohusiana na akaunti za akiba inaweza kuwepo kwa ajili ya malipo ya ada za shule. Jina la mwanafunzi na darasa linaweza kutumika kama kumbukumbu wakati wazazi wanapolipa ada za shule.
- Ada za shule zinazolipwa kwa namna moja – Kutegemeana na mahali shule ilipo, mahitaji na hali ya shule, ada za shule zingeweza kulipwa kwa namna ya chakula, fueli na huduma za shule ikiwa ni pamoja na useremala, upakaji rangi na upaliliaji.
- Malipo kupitia Benki – Akaunti ya shule inaweza kutolewa kwa wazazi ili walipe ada za shule moja kwa moja kwenye akaunti hiyo na slipu za malipo zinaweza kutumwa kwa viongozi wa shule kwa njia ya WhatsApp. Benki zinaweza kutuma taarifa za kila wiki kwa shule kwa ajili ya uchunguzi zaidi kuhusu malipo ya kila wiki.
- Malipo ya ada ya shule kupitia kwa wanafunzi wakubwa – Fedha taslimu/hundi zilizowekwa katika bahasha zenye maelezo yaliyoandikwa kwa uwazi juu ya bahasha hizo zinaweza kupelekwa na wanafunzi wa sekondari za chini na za juu moja kwa moja kwa mamlaka

zinazohusika ambazo zitaandaa stakabadhi zitakazopelekwa na wanafunzi hao kwa wazazi wao.

- Mkopo kwa ajili ya malipo ya ada za shule – Mikopo iliyofanywa na wazazi kwa ajili ya malipo ya ada za shule kutoka katika taasisi mahalia za fedha kama vile MFI, benki za vijijini na huduma nyingine za mikopo inaweza kulipwa moja kwa moja katika akaunti za shule na taasisi za fedha kwa niaba ya wazazi.
- Mifumo ya Benki za Kielektroni – Kulingana na maarifa ya kiteknolojia ya wazazi wa shule, shughuli za benki za kielektroni hujumuisha matumizi ya kadi za benki, uhamishaji wa kimtandao na makato ya moja kwa moja yanaweza kutumiwa na wazazi kulipa ada.

# WAKATI WA KUFUNGUA TENA.

## ANZISHA UTARATIBU RAHISI WA MALIPO KWA WAZAZI AMBAO WAMEPOTEZA KAZI/VYANZO VYAO VYA MAPATO KUTOKANA NA UGONJWA WA KORONA

### Muktadha

Wazazi wengi watakuwa wamepoteza vyanzo vya mapato kutokana na ugonjwa wa korona. Kama taasisi katika jamii ni muhimu uisaidie jamii kurudi katika hali yake ya kawaida na kuwa na utaratibu rahisi zaidi wa malipo ya ada za shule kwa kipindi cha mwanzoni. Hili litakuza taswira yenu kama shule inayojali na utafanya uandikishaji kuwa mkubwa na ukiwawezesha kupata mapato zaidi hapo baadaye.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Hatua unazoweza kuzichukua kuwasaidia wazazi kwa malipo rahisi  ni pamoja na:

- Mipango ya Malipo – Anzisha mipango ya malipo kwa siku, wiki au hata kwa mwezi kwa wazazi  ukizingatia wanavyopenda na uwezo wao.
- Huduma za Shule – Panga na wazazi ambao wangependa kutoa huduma zinazotakiwa kwenye shule ili kulipa ada ya shule kidogokidogo. Lenga kufanya bila ya kuathiri uadilifu wa mzazi na pia kusababisha usumbufu kwa shule.
- Malipo Kidogokidogo – Kwa matukio makubwa, panga kwa ajili ya malipo kidogokidogo ya wazazi kwa tarehe ya baadaye. Wazazi wenye kumbukumbu nzuri za kulipa ada za shule siku za nyuma wanapaswa wawe wadau wakubwa wa kupewa kipindi hiki cha unafuu. Utaratibu/makubaliano rasmi (ya maandishi) yanaweza kuandaliwa kuelezea maafikiano yoyote yaliyofanywa.
- Huduma za Punguzo – Hizi zinaweza kujumuisha punguzo la mara nyingi ambapo wazazi wenye watoto wengi wanaweza kupewa punguzo au wazazi wanalipa mapema ada za watoto wao wanaweza kupewa punguzo mapema. Hili litawahamasisha wazazi kujitahidi kulipa ada.
- Watambulishe wazazi kwenye taasisi za fedha – Wazazi ambao hawawezi kulipa ada kutokana na kupoteza mapato wanaweza kutambulishwa kwenye taasisi za fedha ambazo zinaweza kuwasadia kuwapa mikopo kwa ajili ya matumizi au mikopo ya ada za shule.

# ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE.

| USIMAMIZI WA BIASHARA NA FEDHA | | |
|---|---|---|
| **KABLA YA KUFUNGUA TENA** | | |
| | MHUSIKA | ITAFANYIKA LINI |
| Bainisha njia mbadala za kuongeza mapato tofauti na ada za shule. | | |
| Bainisha njia ambazo unaweza kupunguza gharama za shule ili kuhakikisha kutokwama kwa uendeshaji wa shule. | | |
| Tathmini kiwango chako cha matumizi ya fedha ili kuelewa ni kwa muda gani shughuli za shule zinaweza kuendelea kwa akiba ya fedha zilizopo. | | |
| Hakikisha kuna uwiano wa ada za shule zilizokusanywa. | | |
| Anzisha njia za kukusanya ada za shule wakati ukiendelea kuepuka msongamano mf. kupitia huduma za fedha kwa simu za mikononi. | | |
| Hakikisha au tafuta fedha za kutosha/mtaji wa kazi ili kutekeleza hatua za usafi katika shule. | | |
| **WAKATI WA KUFUNGUA TENA** | | |
| | MHUSIKA | ITAFANYIKA LINI |
| Waunganishe wazazi na taasisi mahalia za fedha kama wateja wa mikopo ya ada za shule ili kuhakikisha ukusanyaji mkubwa wa ada. | | |
| Anzisha njia rahisi za malipo kwa wazazi ambao wamepoteza kazi/vyanzo vyao vya mapato kutokana na ugonjwa wa korona. | | |




# MIKAKATI YA KUELEKEA KUFUNGUA TENA

## Orodhahakiki ya mpango wa kufungua tena shule

## Mazingira Safi na Salama kwa ajili ya Kujifunza

OPPORTUNITY
EduFinance

# MAZINGIRA SAFI NA SALAMA KWA AJILI YA KUJIFUNZA.

| | Kabla ya Kufungua Tena | Wakati wa Kufungua Tena | Baada ya Kufungua Tena |
|---|---|---|---|
| Kuepuka Msongamano | Chunguza hatua ambazo shule inaweza kuchukua kuepuka msongamano. | Badilisha miundombinu/mpango wa madarasa na mabweni ili kurahisisha kuepuka msongamano.<br><br>Hakikisha usafiri wa shule unafuata miongozo ya kuepuka msongamano; fikiria kusitisha huduma za mabasi.<br><br>Fikiria mpango wa awamu za kufungua tena kwa ajili ya shule. | Anzisha tena usafiri wa shule kwa kufuata miongozo ya usafiri salama.<br><br>Fuata maelekezo ya serikali kwa ajili ya kurahisisha kuepuka msongamano. |
| Utaratibu na Uchunguzaji Mpya wa Usafi | Chunguza taratibu zinazohusiana na uvaaji wa barakoa,upimaji wa afya na usafi unaotakiwa na serikali. | Wafundishe wafanyakazi kuhusu utekelezaji wa taratibu za usafi: kuepuka msongamano, kunawa mikono, upimaji wa joto na uvaaji barakoa.<br><br>Endeleza mwongozo wa wazi kuhusu taratibu pale wafanyakazi au wanafunzi wanapokuwa wagonjwa; tenga chumba cha matibabu shuleni.<br><br>Anzisha utaratibu wa mara kwa mara wa uuaji wa vijidudu vya maradhi katika maeneo ya shule. | Simamia utekelezaji wa taratibu na hatua mpya ili kuwafanya wanafunzi kuwa salama. |
| Uelewa | Simamia usambaaji wa ugonjwa wa COVID-19 katika eneo mahalia ambako shule ipo, ikiwa ni pamoja na idadi ya wagonjwa. | Hakikisha wafanyakazi wanafahamishwa vizuri kuhusu COVID -19 ili kuzuia tetesi za uongo na unyanyapaa wowote unaoweza kufanywa kwa wale waliopona. | Simamia usambaaji wa ugonjwa wa COVID-19 ikiwa ni pamoja na miongozo ya kufungwa tena kwa shule, iwapo kutakuwa na kurudia kwa idadi ya maambukizi. |

# KABLA YA KUFUNGUA TENA.

## CHUNGUZA HATUA AMBAZO SHULE INAWEZA KUZICHUKUA ILI KUEPUKA MSONGAMANO

### Muktadha

Katika nchi ambazo shule tayari zimeshafunguliwa tena baada ya kufungwa kutokana na COVID-19, uepukaji wa msongamano unatekelezwa. Ni muhimu kuelewa hatua madhubuti zinazoweza kuanzishwa katika shule yako.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Kiongozi wa shule au mwakilishi wa wafanyakazi anapaswa kufuatilia hatua za kuepuka msongamano ambazo zinaweza kuanzishwa. Kusikiliza maelekezo kutoka serikalini kunaweza kusaidia kutoa ufafanuzi. Hizi ni hatua muhimu au zinazotakiwa kuanzishwa:

- Kufuta au kuahirisha shughuli za baada ya muda wa darasani ambazo hufanywa wakati wa siku za masomo zenye uwezekano mkubwa wa kujichanganya/msongamano. Kama vile elimu ya mazoezi ya viungo, ziara za ugani, kwaya, mkutano, kujifunza kwa vitendo, shughuli za michezo.
- Kupunguza kujichanganya wakati wa usafiri. Hili linaweza kujumuisha uondoaji wa mabasi ya shule, kuepuka matumizi ya usafiri wa umma, kuwahamasisha wazazi kuwapeleka shuleni watoto wao ama kwa miguu au kwa magari yao binafsi.
- Kupunguza urefu wa ratiba. Hili linaweza kujumuisha kuwa na wiki fupi ya kwenda shuleni; siku fupi ya shuleni; wanafunzi kuja kwa kubadilishana siku, kufuta masomo ya asubuhi na usiku.
- Kuondoa matumizi ya maeneo ya pamoja kwa mfano kulia chakula cha mchana madarasani badala ya kumbi za chakula
- Kutekeleza uboreshaji wa sehemu ya kazi kwa wafanyakazi ambako kutafuata hatua za kuepuka msongomano. Hili linaweza kujumuisha kupunguza mikutano ya ana kwa ana au kufuta mikutano, kupunguza kwenda katika ofisi za walimu, kuepuka walimu kusafiri kutoka na kwenda shuleni kwa makundi
- Kuwatenganisha wanafunzi wawapo katika maeneo ya kawaida iwapo uondoaji wa maeneo ya kawaida hauwezekani: Shule inaweza kuamua kwamba wanafunzi wale na wenzao katika chumba cha chakula tu; kuamua wanafunzi wabaki katika sehemu walizopangiwa za eneo la shule.
- Matone ya vitakasamikono na mashine za kupimia joto zipangwe katika geti la shule na kila mtoto apimwe. Hakikisha kwamba upimaji unaendelea, watoto waendelee kukaa umbali wa meta 4 kutoka kwa mwingine.
- Kuzuia wageni: Usiruhusu wazazi au wageni wengine; dhibiti wachuuzi kuingia shuleni.
- Punguza msongamano wakati wa kushusha na kupakia wanafunzi. Ili kufanya hivi:
    1) Panga muda wa familia kuja, zingatia muda tofauti kama inawezekana.
    2) Pale ambapo inawezekana kuchukuliwa na kushushwa kwa mtu kufanywe nje.
    3) Weka alama za kuonekana au vizuizi vya kuelekeza magari na umbali.
    4) Anzisha mfumo wa alama na michakato ya kupunguza mwingiliano wa familia.

## CHUNGUZA HATUA ZINAZOHUSIANA NA UVAAJI WA BARAKOA, UPIMAJI WA AFYA NA USAFI UNAOTAKIWA NA SERIKALI

### Muktadha

Kadri shule zinavyofunguliwa tena, unatakiwa uwe na miongozo iliyo wazi inayotakiwa kutumiwa ambayo itawaongoza wadau mbalimbali kuhusu udhibiti wa COVID-19. Miongozo hii inapaswa kusambazwa na kuwekwa katika maeneo ya shule ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anakumbushwa kuhusu haja ya kujilinda mwenyewe na kuwalinda wengine.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Mara shule zinapofunguliwa tena, timu ya wadau mbalimbali inapaswa kuwa imeandaa miongozo ya usafi & tahadhari shuleni/sera zilizotoka katika miongozo ya idara mbalimbali za serikali kama vile Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu kuhusu COVID-19 kwa namna rahisi na kutafsiriwa ama katika lugha ya eneo lile au katika vielelezo.

Miongozo hii itasambazwa kwenye jumuiya ya shule kabla ya shule kufunguliwa tena ili kuhakikisha:

1. Wanajiandaa vema mapema kwa ajili ya mahitaji yanayotakiwa kama vile aina ya barakoa zinazopendekezwa, au mahitaji ya kunawa mikono yanayotakiwa/kutolewa mf. sabuni au maji.
2. Wanatenganisha muda wa shule na kuhamasisha ujifunzaji wa masafa pale inapobidi
3. Wanaiga tabia/taratibu mpya zilizoanzishwa na shule kuhusu miongozo ya usalama

Hakikisha kwamba MST inaongoza katika kutafiti na kuwaelewesha wafanyakazi wa shule, wazazi, wanafunzi na wageni kufuata miongozo iliyowekwa shuleni kama ilivyoshauriwa na serikali. Zifuatazo ni hatua zinazopaswa kuchukuliwa:

- Sambaza taarifa zilizo wazi na sahihi kuhusu COVID-19 – bila ya kuingiza woga na wasiwasi bali kuhamasisha tahadhari binafsi kwa wadau wote wa shule
- Timu ya uwajibikaji ndani ya shule kama vile viranja na walimu – timu ambayo itahakikisha kuwa jumuiya ya shule inafuata miongozo na kuitikia dharura kwa wakati.
- Sheria iliyo wazi ya kutomruhusu mtu asiye na barakoa shuleni – MST ihakikishe kwamba wale wote wanaokwenda katika mazingira ya shule wanavaa barakoa
- Fanya maboresho ya utoaji wa huduma za Maji, Afya na Usafi –ongeza idadi ya marudio ya kufanya usafi na kuua vijidudu vya maradhi shuleni, boresha udhibiti taka na kuwa na vituo vya kunawa mikono pamoja na hatua za jinsi ya kunawa mikono.
- Programu za chakula hasa kwa wale wanaotoka nje au wanaoleta chakula shuleni – shule ama itoe chakula ili kuepuka magari mengi ya watoa huduma/wazazi wakati wa saa za shule au kuja na programu ya chakula inayohusiana na usafi wakati chakula kinapoletwa shuleni.

# WAKATI WA KUFUNGUA TENA.

## BADILI MIUNDOMBINU/MPANGILIO WA MADARASA NA MABWENI ILI KUHAKIKISHA UEPUKAJI WA MSONGAMANO

### Muktadha

Moja ya hatua ya kwanza ambayo shule inapaswa kuichukua wakati inapanga kufungua tena ni kubadilisha miundombinu ya darasa ili kuhakikisha kwamba ufundishaji na ujifunzaji unaweza kuanza bila ya hatari ya wanafunzi kupatwa na ugonjwa. Fikiria kile ambacho ungetarajiwa kukifanya ili ufanye mabadiliko haya na ni walimu/wafanyakazi gani ambao ungewapangia majukumu hayo.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Yafuatayo ni mabadiliko ambayo yanaweza kuwa ya muhimu katika shule yako:

- Punguza/minnya idadi ya watoto katika madarasa. Geuza vyumba visivyotumiwa/visivyo na kitu/vya ziada au maeneo ya wazi kuwa madarasa.
- Fikiria mipangilio ya kulala katika mabweni – je, vitanda vya chini na juu vinakubalika, wanafunzi walale katika kitanda kimojakimoja?
- Rekebisha matumizi ya vyoo, hasa wakati wa mapumziko ya chakula cha mchana. Wakati hili ni gumu kutekeleza, ni muhimu kuendelea kuepuka msongamano katika maeneo ya pamoja kama vile vyoo vya shule. Hili linaweza kuhitaji shule kupanga muda tofauti wa kupumzika kwa madarasa tofauti ili kupunguza msongamano katika vyoo.
- Kuendelea kuwa na umbali unaoshauriwa kati ya wanajumuiya wa shule (kila serikali inashauri idadi fulani ya meta) anzisha alama wanaposimama watoto wakati wanapojipanga mistari kama vile foleni za chakula cha mchana.
- Tumia maeneo ya nje kwa ajili ya kusomea kwa kuanzisha madarasa ya nje.
- Ndani ya darasa panga tena madawati ili kuongeza nafasi, waambie wanafunzi wabaki wamekaa darasani na yapange madawati kuangalia katika uelekeo mmoja (badala ya kuwa yanaangaliana) ili kupunguza maambukizo yanayosababishwa na virusi vinavyotokana na matone (mf. kutokana na kuzungumza, kukohoa, kupiga chafya).

## ZINGATIA MPANGO WA AWAMU YA KUFUNGUA TENA SHULE

### Muktadha

Kutokana na ukali wa ugonjwa wa korona katika eneo lako mahalia, viongozi wa shule hawataweza kuanza madarasa kwa wanafunzi wote wakati wa kufungua tena. Katika matukio hayo, shule iangalie kwanza mpango wa kuufungua tena kwa awamu, kabla ya kurudisha shughuli zote za shule

### Utekelezaji katika Shule Yako

Kuna njia nyingi mbadala ambazo viongozi wa shule wanaweza kuzichagua wakati wakifikiria mpango wa kufungua tena shule kwa awamu.

- Kanuni ya namba shufwa na witiri: Nusu ya madarasa waje shuleni katika tarehe zenye namba witiri katika mwezi, ambapo nusu nyingine waje shuleni katika tarehe zenye namba shufwa katika mwezi
- Ratiba ya asubuhi na jioni: Yagawe madarasa katika mikondo miwili. Mkondo mmoja uje asubuhi na mkondo mwingine uje jioni. Hili linaweza kuwahitaji viongozi wa shule kupunguza saa za kufundisha kwa kila darasa linalokuja shuleni
- Madarasa yanayofanya mitihani ya taifa: Shule zinaweza kuanza uendeshaji kwa kuyaita madarasa yanayofanya mitihani ya taifa tu kwa wakati huo. Usomaji wa nyumbani unaweza kuendelea kwa madarasa yaliyobaki mpaka idadi ya wagonjwa katika eneo/mkoa itakapokuwa ya kawaida/itakapopungua, ndipo shule inaweza kurudisha madarasa yote.
- Mchanganyiko wa ujifunzaji wa nyumbani na wa ana kwa ana: Shule inaweza kuwataka wanafunzi kuja kwa ajili ya kufundishwa sehemu maalumu ya muhtasari, ambapo sehemu ziingine wanafunzi wanaweza kufundishwa kwa masafa.

## ENDELEZA MWONGOZO MZURI WA TARATIBU IWAPO WAFANYAKAZI AU WANAFUNZI WATAKUWA WAGONJWA; TENGA CHUMBA CHA MATIBABU SHULENI

### Muktadha

Ili kuhakikisha kuwa shule yako inaweza kubaki wazi na kuendelea kuaminiwa na wazazi ili walete watoto wao shuleni ni muhimu kuwa na mwongozo mzuri wa nini kifanyike pale wafanyakazi au wanafunzi wanapokuwa wagonjwa.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Wasiliana na wafanyakazi na wazazi kuwa hakuna mtu anayeruhusiwa kuja shuleni iwapo ana dalili zozote za COVID-19. Shirika la Afya Duniani (WHO) linasambaza dalili hizo. Dalili za kawaida zaidi ni:

- Homa
- Kikohozi kikavu
- Uchovu

Pia kwa kuzingatia Miongozo ya WHO au ya kitaifa, panga muda ambao wanafunzi wanapaswa wasije shuleni.

Kwa wale ambao wataumwa wakati wa siku ya shule kunapaswa kuwe na sehemu ya shule ambayo imepangwa kama chumba kilichoandaliwa kwa ajili ya tiba, ambapo wanafunzi na wafanyakazi wanaweza kutengwa na wengine.

Vilevile:

- Endesha tathmini ya vihatarishi kwa wafanyakazi na wanafunzi wote – wale wenye dalili za awali/ugonjwa.
- Hakiki na imarisha uhusiano na mawakala wa rufaa na sambaza mawasiliano ya dharura – iwapo kutakuwa na dharura ya COVID.

# ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE.

| MAZINGIRA SAFI NA SALAMA KWA AJILI YA UJIFUNZAJI | | | |
|---|---|---|---|
| KABLA YA KUFUNGUA TENA | | Fikiria mpango wa kufungua tena shule kwa awamu. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI |
| Chunguza hatua ambazo shule inaweza kuchukua kuepuka msongamano. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | | |
| Chunguza taratibu zinazohusiana na uvaaji wa barakoa,upimaji wa afya na usafi unaotakiwa na serikali.. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | Wafundishe wafanyakazi kuhusu kutekeleza taratibu za usafi shuleni: kuepuka msongamano, kunawa mikono, upimaji joto na uvaaji wa barakoa. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI |
| Dhibiti ueneaji wa ugonjwa wa COVID -19 katika eneo mahali shule ilipo, ikiwa ni pamoja na wagonjwa. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | Endeleza mwongozo mzuri kuhusu taratibu pale wafanyakazi au wanafunzi wanapokuwa wagonjwa; tenga chumba cha matibabu shuleni. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI |
| WAKATI WA KUFUNGUA TENA | | Panga uuaji wa vijidudu vya maradhi katika maeneo ya shule. | MHUSIKA |
| Badilisha miundombinu/mpangilio wa madarasa na mabweni ili kuhakikisha uepukaji wa | MHUSIKA | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| msongamano. | ITAFANYIKA LINI | | ITAFANYIKA LINI |
| Hakikisha usafiri wa shule unafuata miongozo ya uepukaji msongamano; Fikiria kusitisha huduma za mabasi. | MHUSIKA | Hakikisha wafanyakazi wamepewa taarifa ya kutosha kuhusu COVID-19 ili kuzuia tetesi za uongo na unyanyapaa wowote unaohusishwa na wale waliopona. | MHUSIKA |
| | ITAFANYIKA LINI | | ITAFANYIKA LINI |




# MIKAKATI YA KUELEKEA KUFUNGUA TENA

## Orodhahakiki ya mpango wa kufungua tena shule

### Kufundisha na Kujifunza

OPPORTUNITY
EduFinance

# KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA.

| | Kabla ya Kufungua Tena | Wakati wa Kufungua Tena | Baada ya Kufungua Tena |
|---|---|---|---|
| Mitaala | Simamia na fuata mwongozo kutoka serikalini kuhusiana na mabadiliko yoyote katika mitaala na ratiba ya mitihani.<br><br>Watumie wazazi orodha ya mada zilizofundishwa wakati shule zilipofungwa na waombe wachague mada zilizokamilishwa na mtoto wao nyumbani. | Fanya ustawi wa wafanyakazi kuwa kipaumbele. Wape muda kurekebisha upya shule, toa madarasa ya msasa iwapo yatahitajika na wasikimbilie katika kufundisha mtaala wote.<br><br>Panga muda kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi kuhusu taratibu mpya ambazo shule imezianzisha ili kuwafanya kuwa salama.<br><br>Punguza mtaala kwa ajili ya muda uliobaki wa mwaka wa masomo kwenda kwenye ngazi inayofikiwa, ukiweka kipaumbele mada ambazo zinafaa zaidi. | Fikiria jinsi wanafunzi wanavyoweza kushika mafunzo waliyokosa pale shule ilipokuwa imefungwa. Lenga hasa kuhusu ngazi za kusoma, kuandika na kuhesabu. |
| Kujifunza Nyumbani | Bainisha chaneli kwa shule yako kutoa mafunzo ya nyumbani kama vile alama zilizokosekana, WhatsApp, Facebook, ujumbe mfupi wa maandishi na Zoom.<br><br>Wafundishe wafanyakazi jinsi ya kufundisha kwa kutumia chaneli za mafunzo ya nyumbani, hakikisha mafunzo yanafuata na kujenga ujifunzaji wa sasa shuleni.<br><br>Tuma vitinivilivyochapishwa na vifaa saidizi kwa wanafunzi ambao wazazi wao hawana simu za kisasa au intaneti. | Panga kwa ajili ya uwiano wa ufundishaji wa mtu na ujifunzaji wa nyumbani iwapo wanafunzi hawatarudi shuleni kwa muda wote au kama muda wa shule umepunguzwa. | Andaa kwa ajili ya ufungaji shule wa baadaye kwa kuongeza uwezo wa shule kuchangia masomo kimasafa. Hili linaweza kujumuisha kuanzisha tovuti ya shule. |

# KABLA YA KUFUNGUA TENA.

## SIMAMIA NA FUATA MWONGOZO KUTOKA SERIKALINI KUHUSU MABADILIKO YOYOTE KATIKA MTAALA NA RATIBA ZA MITIHANI

### Muktadha

Shule nyingi hazijawahi kufuata kanuni za msingi ili kuhakikisha mazingira yanayofaa zaidi kwa ajili ya kujifunza. Ushirikishwaji wa walimu katika kufanya uamuzi ni mdogo. Kuna msukumo kwa madarasa ya wanaomaliza kukamilisha mihitasari. Kujifunza nyumbani/kwa masafa ni kitu kingine ambacho kinatekelezwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ugonjwa wa virusi vya korona

### Utekelezaji katika Shule Yako

- Kuna haja ya kutarajia kile ambacho serikali inaweza kutoa kama masharti kwa ajili ya shule kufunguliwa tena
- Zingatia kuangalia miongozo ya WHO/UNICEF
- Rejea katika mahitaji ambayo tayari yameanzishwa ya viwango vya chini kwa shule kuwa na mazingira mazuri ya ujifunzaji.
- Wajumuishe wadau wa shule hasa walimu na wazazi kwa ajili ya mashauriano kuhusu kipi kinaweza kuwa bora kwa ajili ya mustakabali mzuri.
- Ilete kwenye bodi ya walimu ili kuanzisha ufunguaji mzuri wa mpango wa muhula
- Fikiria kutoa msaada wa kimhemko zaidi kwa wanafunzi na kujumuisha zaidi PSHE katika mtaala
- Anzisha mpango wa kuendelea na ujifunzaji wa nyumbani, hasa kwa madarasa yenye mitihani
- Anzisha mfumo ambao una mwitikio mzuri na wa kawaida kutoka kwa wanafunzi na wazazi

## WATUMIE WAZAZI ORODHA YA MADA ZILIZOFUNDISHWA WAKATI SHULE ZILIPOFUNGWA NA WAOMBE WACHAGUE MADA ZILIZOKAMILISHWA NA MTOTO WAO NYUMBANI

### Muktadha

Wanafunzi wote hawatakuwa na mazingira yanayofaa ya ujifunzaji nyumbani. Hii ina maana kuwa kutakuwa na tofauti katika ngazi za ujifunzaji wakati wanafunzi watakaporudi shuleni. Kusaidia ustawi wa mwanafunzi, viongozi wa shule wanahitaji kutathmini ngazi za ujifunzaji wa kila mwanafunzi wakati watakaporudi shuleni, ili shule iweze kurekebisha ipasavyo mtaala na ratiba yake.

### Utekelezaji katika Shule Yako

- Andaa orodha ndefu ya mada, vitini na kazi ambazo zimesomwa na wanafunzi wakati shule zilipofungwa.
- Tuma orodha hiyo kwa wazazi wote kwa kutumia whatsapp kabla ya shule kufunguliwatena. Kiongozi wa shule pia anaweza kuichapisha orodha hiyo na kuituma kwa wazazi ambao hawana simu za kisasa.

- Waombe wazazi kurudisha shuleni mada ambazo zimekamilishwa katika usimamizi wao kabla ya tarehe ya kufugua tena.
- Kwa kutumia matokeo, bainisha ni mada zipi zilizokamilishwa na wengi, ambazo wanafunzi wanahitaji madarasa ya msasa kuhusiana na mada ambazo hazijakamilishwa.

## BAINISHA CHANELI KWA AJILI YA SHULE YAKO ILI KUTOA MAFUNZO YA NYUMBANI KAMA ALAMA ZILIZOKOSEKANA, UJUMBE MFUPI WA MAANDISHI, WHATSAPP NA FACEBOOK

### Muktadha

Wakati shule zimefungwa ni muhimu kuendelea kuwasaidia wanafunzi na wazazi wao kwa kuwapatia kazi za kufanya nyumbani. Hili litakuwa na faida nyingi za:

- Kuonyesha shule zinawajibika kwa wanafunzi
- Wanafunzi na wazazi kuendelea kujihusisha na shule na kutaka zaidi kujiandikisha wakati wa kufungua tena shule
- Walimu kuwa na shughuli za kufanya na kubaki wakijishughulisha kikamilifu na shule
- Kuunda njia za kiubunifu kwa walimu kufanya kazi kwa masafa na wanafunzi hata baada ya kuisha kwa ugonjwa wa korona
- Wanafunzi kuendelea na shughuli za kitaaluma

### Utekelezaji katika Shule Yako

Bainisha njia za kutoa mafunzo ya nyumbani ambazo zitakuwa bora kuweza kuwafikia wazazi wengi kadri iwezekanavyo. Zifuatazo ni njia ambazo unaweza kuzifikiria:

Sehemu za kupeleka, kuchukua – baadhi ya viongozi wa shule wameandaa mahali pa kuchukulia ambapo nakala halisi za kazi zinaweza kuchukuliwa katika njia ya masafa katika jamii. Hili linahitaji uwezo wa kuchapisha kazi katika bechi na ushirikiano na walimu ili kutoa kazi zilizo tayari.

Ujumbe mfupi wa maandishi – kwa wazazi ambao hawawezi kupata intaneti au simu za kisasa, huduma ya ujumbe mfupi wa maandishi inatoa njia ya kuwasiliana nao. Kazi zilizopendekezwa au ratiba inayotakiwa kusambazwa katika namna rahisi na ya wazi kulingana na idadi ya tarakimu za ujumbe mfupi zinazoweza kutumwa ambazo zina ukomo.

WhatsApp – mwalimu anaweza kuandaa kundi la WhatsApp ambalo linajumuisha wazazi wa darasa au madarasa ambayo anayafundisha. Wazazi wanaweza kushiriki mazoezi haya na wanafunzi wao. WhatsApp inawaruhusu walimu kuwa wabunifu zaidi badala ya kutuma ujumbe mfupi tu. Walimu wanaweza kutumia kamera iliyo katika simu kusambaza kazi zilizoandikwa kwa mkono au ratiba za kila wiki. Walimu wanaweza kurekodi vipande vya kusikiliza kama vile jaribio la kufanya hesabu kwa kichwa au jaribio la matamshi.

Facebook – shule inaweza kuwa na ukurasa wa Facebook au kurasa binafsi za darasa ambapo kazi inaweza kutumwa. Kurasa hizi ni rahisi kuandaliwa na rahisi kwa ujifunzaji wa kusambaza picha za nyaraka.

Tovuti – tovuti ya shule ni sehemu nzuri ya kusambaza kazi kwa wanafunzi kwa shule ambazo wameiunda. Nyongeza ya kurasa za tovuti zinaweza kuundwa ambapo kazi za madaraja mbalimbali (makundi ya mwaka) zinaweza kusambazwa.

### WAFUNDISHE WAFANYAKAZI JINSI YA KUTUMIA CHANELI ZA MAFUNZO YA NYUMBANI, HAKIKISHA MAFUNZO YANAFUATA NA KUJENGA UJIFUNZAJI WA KISASA SHULENI

#### Muktadha

Ili mafunzo ya nyumbani yawe yenye ubora mtu (kwa kawaida mwalimu) anayetoa vitini kwa wazazi anahitaji kujua jinsi ya kutumia teknolojia yoyote kwa ufanisi. Wanapaswa kufuata mtaala wa taifa ili mafunzo ya nyumbani yajengwe katika ujifunzaji ambao ulikuwa unafanywa kabla ya shule kufungwa.

#### Utekelezaji katika Shule Yako

Wafundishe walimu jinsi ya kutumia teknolojia yoyote ili watoe mafunzo ya nyumbani. Unaweza kuwa na baadhi ya walimu ambao wazuri zaidi ya wengine katika kufanya kazi kwa njia hii. Ungeweza kuwapanga walimu katika jozi ili kutoa msaada au kuwa na kundi la kupiga kwa WhatsApp ambapo mpaka walimu 8 wanaweza kushirikishwa katika mafunzo kwa wakati huohuo.

Mara chaneli ya mafunzo ya nyumbani inapokamilika, ni muhimu kuweka miongozo kwa ajili ya walimu kuhusu mafunzo ya nyumbani. Utoaji wa mambo mengi au machache sana ya kujifunza hautakuwa na tija. Amueni kama shule kiasi cha maudhui ambacho kitafaa kwa ajili ya mafunzo ya nyumbani – haya yanaweza kuwa pungufu ya kiasi cha ujifunzaji ambacho kinaweza kufikiwa darasani. Vilevile, angalieni mahitaji ya upimaji wa kazi. Je, wazazi watakuwa wanatuma kazi za wanafunzi ili zisahihishwe au walimu watasambaza majibu ili wazazi na wanafunzi waweze kusahihisha kazi wakiwa nyumbani?

# WAKATI WA KUFUNGUA TENA.

### FANYA USTAWI WA MWANAFUNZI KUWA KIPAUMBELE WAKATI WANAFUNZI WANAPORUDI SHULENI. WAPATIE MUDA WA KUJIWEKA SAWA NA USIKIMBILIE KUWAFUNDISHA MTAALA WOTE

#### Muktadha

Kutokana na mapumziko marefu ambayo wanafunzi wamepata, kunaweza kuwe na mabadiliko mengi ya kitabia wakati shule inapofunguliwa tena. Wanafunzi watahitaji muda wa kutosha kujiweka sawa tena kikamilifu katika mfumo wa shule. Wiki chache za mwanzo zitakuwa muhimu kwa ajili ya makuzi ya kiakili kwa mwanafunzi na hivyo itakuwa muhimu kulenga katika ustawi na hali nzuri ya ustawi wa akili kwa wanafunzi.

#### Utekelezaji katika Shule Yako

Mara shule itakapofunguliwa tena na wanafunzi kuanza kwenda madarasani, unaweza kutaka kuzingatia mambo yafuatayo:

- Fikiria marekebisho ya ratiba – Kutokana na mapumziko marefu, baadhi ya stadi za kielimu zinaweza kupungua na uelewa na utambuzi unaweza kuchukua muda. Fikiria kupunguza masomo kwa kiwango na kubakiwa na manne kwa siku na ongeza muda wa ziada wa

masomo yenye mahesabu ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kikamilifu dhana wanayofundishwa. Kwa wanafunzi wanaotakiwa kufanya mitihani ya taifa, unaweza kuendeleza ratiba iliyopo lakini kuwa makini na hali yao na wafanye wapate urahisi katika maandalizi ya mitihani yao hatua kwa hatua.

- Anzisha Elimu Binafsi, Elimu Jamii na Elimu Afya (PSHE) – Chagua walimu wachache na wawafundishe wanafunzi kuhusu PSHE. Hili litawasaidia wanafunzi kushirikishana hofu zao na walimu na kurudi katika hali ya kawaida. Somo la PSHE litawasaidia wanafunzi kuwaandaa kiakili kwa ajili ya mtaala mzima.
- Tumia muda wa nje na wanafunzi– Anzisha vipindi vichache vya nje ya darasa na wanafunzi. Waambie wakae kimduara na wenzao na mwalimu nje ya darasa na washirikishane uzoefu binafsi walioupata walipokuwa nje ya shule. Hili litawasaidia kupunguza woga na wasiwasi wao katika darasa kuhusu mfumo mpya.
- Jihusishe na shughuli mbalimbali – Katika wiki chache za mwanzo, ongeza katika mtaala njia za kujifunza kwa vitendo zaidi. Anzisha ujengaji wa timu na shughuli za vitendo kama vile klabu za kusoma au matamshi. Hakikisha kwamba shughuli zote zinafuata miongozo ya uepukaji wa msongamano iliyowekwa na shule
- Anza kwa upitiaji tena wa dhana zilizofundishwa zamani – Pima uelewa wa mada zilizofundishwa nyuma, kwa hisabati itakuwa ni upitiaji tena wa matumizi ya njia za ukokotoaji ili kuona kile ambacho wanafunzi wanaweza kufanya sasa kabla ya kwenda kwenye mafunzo mengine.

## WEKA UWIANO WA KUFUNDISHWA ANA KWA ANA NA MAFUNZO YA NYUMBANI IWAPO WANAFUNZI HAWATARUDI SHULENI KWA MUDA WOTE

### Muktadha

Wakati shule zitakapofunguliwa tena kunaweza kuwa na mabadiliko yanayotakiwa katika ratiba ya shule ili kuruhusu uepukaji wa msongamano. Madarasa yanaweza kugawanywa ambapo wanafunzi wengine watakuwa wanakwenda asubuhi au mchana. Baadhi ya madarasa yanaweza kuendeshwa kwa baadhi ya siku za wiki tu. Pia kunaweza kuwa na uwezekano wa kufungwa shule hapo baadaye. Iwapo hili litatokea mafunzo ya nyumbani yataendelea kuwa ya muhimu.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Mara ratiba kwa kila daraja (kundi la mwaka) zitakapothibitishwa, anzisha miongozo mipya kwa walimu kuhusu mafunzo ya nyumbani:

- Panga mahitaji kwa mafunzo ya nyumbani – haya yatajumuisha kiasi cha kazi ambazo walimu wanatarajiwa kupanga kwa ajili ya mafunzo ya nyumbani, masomo ambayo yatapewa kipaumbele na jinsi kazi zinavyopaswa kuhusishwa na ujifunzaji wa darasani.
- Toa ratiba ya mafunzo ya nyumbani – Ratiba itawasaidia wazazi na wanafunzi kuona kwa uwazi kinachotarajiwa kwa kila siku.
- Baini kiwango cha msaada ambacho walimu watakitoa kimasafa – Je, walimu watakuwepo kwa maswali kutoka kwa wazazi? Je, kutakuwa na darasa la kundi la WhatsApp ambapo walimu wanaweza kutoa ushauri na mrejesho? Je, walimu watawaita wazazi kila wiki ili kujadili matarajio?
- Amua jinsi kazi itakavyosahihishwa – Wanafunzi watapewa majibu na kusahihisha kazi zao wenyewe au walimu watasahihisha kazi zitakaporudishwa. Labda mchanganyiko wa njia zote mbili utatumiwa.

# ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE

<table>
<tr><th colspan="4">KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA</th></tr>
<tr><th colspan="2">KABLA YA KUFUNGUA TENA</th><th colspan="2">WAKATI WA KUFUNGUA TENA</th></tr>
<tr><td rowspan="2">Simamia na fuata mwongozo kutoka serikalini unaohusu mabadiliko yoyote katika mtaala na ratiba za mitihani</td><td>MHUSIKA</td><td rowspan="2">Fanya ustawi wa mwanafunzi kuwa kipaumbele. Wape muda wa kujiweka sawa upya katika shule na usikimbilie kuwafundisha mtaala wote</td><td>MHUSIKA</td></tr>
<tr><td>ITAFANYIKA LINI</td><td>ITAFANYIKA LINI</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Watumie wazazi orodha ya mada zilizofundishwa wakati wa kufungwa kwa shule na waombe wachague mada zilizokamilishwa na mtoto wao nyumbani</td><td>MHUSIKA</td><td rowspan="2">Panga muda wa kuwafundisha wanafunzi kuhusu utaratibu mpya ambao shule imeuanzisha ili kuwafanya wawe salama</td><td>MHUSIKA</td></tr>
<tr><td>ITAFANYIKA LINI</td><td>ITAFANYIKA LINI</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Bainisha chaneli kwa ajili ya shule yako kutoa mafunzo ya nyumbani kama vile sehemu za alama zilizokosekana, WhatsApp, Facebook, ujumbe mfupi wa maandishi na Zoom</td><td>MHUSIKA</td><td rowspan="2">Punguza mtaala kwa ajili ya mwaka wa shule uliobaki kuwa katika ngazi inayofikika, weka kipaumbele mada ambazo ni muhimu zaidi</td><td>MHUSIKA</td></tr>
<tr><td>ITAFANYIKA LINI</td><td>ITAFANYIKA LINI</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wape mafunzo wafanyakazi kuhusu namna ya kutumia chaneli za mafunzo ya nyumbani, hakikisha mafunzo yanafuata na kujengwa katika ufundishaji uliopo shuleni | MHUSIKA | Weka uwiano wa ufundishaji wa ana kwa ana na mafunzo ya nyumbani iwapo wanafunzi hawatarudi shuleni kwa muda wote | MHUSIKA |
| | ITAFANYIKA LINI | | ITAFANYIKA LINI |
| Tuma vitini vya mazoezi na vilivyochapwa na vifaa saidizi kwa wanafunzi ambao wazazi wao hawana simu za kisasa au intaneti | MHUSIKA | | |
| | ITAFANYIKA LINI | | |




# MKAKATI WA KUELEKEA KUFUNGUA TENA

## Orodhahakiki ya mpango wa kufungua tena shule

## Ushirikishwaji wa Wazazi

OPPORTUNITY
EduFinance

# USHIRIKISHWAJI WA WAZAZI.

| | Kabla ya Kufungua Tena | Wakati wa Kufungua Tena | Baada ya Kufungua Tena |
|---|---|---|---|
| Taarifa ya Mawasiliano | Weka taarifa zote za mawasiliano ya wazazi pamoja ili wazazi wote waweze kupatiwa taarifa katika kipindi cha zuio la kutotoka nyumbani. | Kusanya taarifa za mawasiliano ya sasa kwa wazazi wowote ambao shule imeshindwa kuwafikia wakati wa mfungo. | Panga kuhuisha taarifa za mawasiliano ya wazazi mara kwa mara. |
| Mawasiliano | Hakikisha unaendeleza mawasiliano ya mara kwa mara na wazazi; wafahamishe kuhusu hatua zinazochukuliwa kuwasaidia wanafunzi na kuifanya shule kuwa salama. | Panga kwa ajili ya uhamasishaji wa jumuiya, ukisisitiza umuhimu wa kurudi tena shuleni.<br><br>Wataarifu wazazi kuhusu tarehe ya kufungua tena na sheria zinazohusu nani aje shuleni, ikiwa ni pamoja na madarasa gani yatarudi (iwapo kuna awamu za kufungua tena). | Endelea kuwataarifu wazazi kuhusu hatua ambazo shule inazichukua kuzuia ueneaji wa COVID-19; hii itasaidia kuendelea kuandikisha wanafunzi. |

# WAKATI WA KUFUNGUA TENA.

## WATAARIFU WAZAZI KUHUSU TAREHE YA KUFUNGUA TENA NA SHERIA ZINAZOHUSU NANI AJE SHULENI IKIWA NI PAMOJA NA MADARASA GANI YATARUDI (IWAPO KUNA AWAMU ZA KUFUNGUA TENA).

### Muktadha

Viongozi wa shule wanapaswa kuwataarifu wazazi tarehe za kufungua tena na hatua ambazo shule itazichukua wakati wa kufungua tena, ili kuhakikisha kwamba wazazi wamejiandaa vizuri na wamewaandaa mapema watoto wao kufikia matarajio ya shule. Hili litahakikisha kwamba ratiba mpya ya shule haitokei kama kitu cha kushangaza kabisa kwa watoto na kuwasaidia kujiweka sawa na mabadiliko

### Utekelezaji katika Shule Yako

Wakati wa kuandaa mpango wako wa kufungua tena shule, mara unapokuwa umepanga tarehe na sheria zinazohusiana na kufungua tena, tafadhali hakikisha kwamba taarifa inatolewa kwa wazazi wote. Hili litawahitaji viongozi wa shule:

- Kupanga tarehe ya kufungua tena shule kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya/Wizara ya Elimu katika maeneo yao yanayohusika

- Kuandaa mpango kwa ajili ya kufungua tena ambao unaruhusu utekelezaji wa hatua za kuepuka msongamano. Mpango wa kufungua tena unaweza kuruhusiwa kwa ajili ya ufunguaji tena mzima au wa awamu kutegemea na uzito wa ugonjwa wa korona katika eneo/ukanda husika.
- Shule zingeweza kufikiria kutekeleza sheria ya namba witiri na shufwa, kwa kuanzisha bechi mbili- ambapo nusu ya madarasa kuja shuleni asubuhi na nusu jioni au kwa kuanzia shule iwaite wanafunzi ambao watafanya mitihani ya taifa na baadaye kuwaita wanafunzi wengine waliobaki
- Shule iwafahamishe wazazi wasiwalete watoto wao iwapo wataonyesha dalili za COVID-19 au wamekutana na mtu aliyeathiriwa na COVID-19.
- Kwa kuzingatia mapendekezo kutoka katika mamlaka mahalia, shule zinaweza kuwataka wazazi kuwaleta watoto wao shuleni wakiwa na barakoa na glavu.

## PANGA KWA AJILI YA UHAMASISHAJI WA JUMUIYA UKISISITIZA UMUHIMU WA KURUDI SHULENI

### Muktadha

Kutokana na familia kupata matatizo ya kifedha wakati shule na biashara zilipofungwa hakikisha wanafunzi wote wanaoandikishwa tena watakuwa kipaumbele kwa shule. Kwa kawaida katika hali kama hizi wanafunzi ambao si kawaida yao kutofika shule, hasa wasichana, wanaweza kushindwa kuja shuleni. Ni muhimu shule ifanye kazi ya kuihamasisha jumuiya kuhusu umuhimu wa kurudi shuleni.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Uhamasishaji wa jumuiya yako ulenge katika kuwasaidia wanafunzi kurudi shuleni hasa wasichana, ikiwa ni pamoja na wasichana wenye ujauzito ambao walikuwa nje ya shule kabla ya shule kufungwa kutokana na ugonjwa wa korona.

Panga kampeni ya Kurudi Shuleni kwa kutumia ujumbe kwa ajili ya jumuiya kuwashawishi na kuwasaidia kwa bidii wanafunzi kurudi shuleni. Wasiliana vizuri na jumuiya pindi tarehe ya kufungua tena shule itakapokuwa imepangwa. Jumuisha katika ujumbe wako:

- Kwa nini kusoma ni muhimu sana kwa ajili ya maisha ya baadaye ya wanafunzi.
- Hatua ambazo shule inazichukua kuwafanya wanafunzi wawe salama (kunaweza kuwa na woga wa kurudi baada ya kuishi chini ya zuio la kutotoka nyumbani). Hizi zitajumuisha usafi na kunawa maji, ambapo wafanyakazi wamepewa mafunzo kuhusu hatua zinazohitajika kuwafanya wanafunzi kuwa salama.

Wakati shule zinapofungliwa tena, timu ya viongozi waandamizi na PTA wasimamie mahudhurio ya wanafunzi hasa wasichana na wachukue hatua kuwasiliana na wale ambao hawajarudi au hawafiki kila siku.

# ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE

| USHIRIKISHWAJI WA WAZAZI | | | |
|---|---|---|---|
| KABLA YA KUFUNGUA TENA | | WAKATI WA KUFUNGUA TENA | |
| Weka taarifa zote za mawasiliano ya wazazi pamoja ili wazazi wote waweze kupatiwa taarifa katika kipindi cha zuio la kutotoka nyumbani. | MHUSIKA | Kusanya taarifa za mawasiliano za sasa kwa wazazi wowote ambao shule imeshindwa kuwafikia wakati wa kufungwa. | MHUSIKA |
| | ITAFANYIKA LINI | | ITAFANYIKA LINI |
| Uwe na mawasiliano ya mara kwa mara na wazazi; wataarifu kuhusu hatua zitakazochukuliwa kuwasaidia wanafunzi na kuifanya shule iwe salama | MHUSIKA | Panga kuihamasisha jumuiya ukisisitiza umuhimu wa kurudi shuleni | MHUSIKA |
| | ITAFANYIKA LINI | | ITAFANYIKA LINI |
| | | Wataarifu wazazi tarehe ya kufungua tena shule na sheria zinazohusiana na nani atakayekuja shuleni, ikiwa ni pamoja na madarasa gani yatakayorudi | MHUSIKA |
| | | | ITAFANYIKA LINI |



# MIKAKATI YA KUELEKEA KUFUNGUA TENA

## Orodhahakiki ya mpango wa kufungua tena shule

## Ushirikishwaji wa Wafanyakazi

OPPORTUNITY EduFinance

# USHIRIKISHWAJI WA WAFANYAKAZI

| | Kabla ya Kufungua Tena | Wakati wa Kufungua Tena | Baada ya Kufungua Tena |
|---|---|---|---|
| Msaada na Mawasiliano | Wasiliana na wafanyakazi kila siku kuhakikisha wako salama na wanaendelea vema. Ikiwezekana toa msaada wa unasihi.<br><br>Hakikisha mawasiliano ya kila wakati na walimu kuhusu mabadiliko katika utaratibu wa malipo. | Hakikisha malipo ya mishahara ya walimu yanaendelea na kufanyika kwa wakati, hususani kwa wale wenye mikataba isiyotabirika, ili kusaidia ubakiaji na ustawi wa mwalimu. | |
| Mahudhurio ya Wafanyakazi | Hakiki sera ya mahudhurio ya wafanyakazi ili kujumuisha kutohudhuria kutokana na sababu za kiafya. | Panga kwa ajili ya uwezekano wa kupunguza wafanyakazi kutokana na walimu kutorudi kwa sababu za kiafya au kifedha; panga kupitia upya ratiba ya wafanyakazi na ajiri wafanyakazi wapya. | |

# KABLA YA KUFUNGUA TENA.

## WASILIANA NA WAFANYAKAZI MARA KWA MARA ILI KUHAKIKISHA WAKO SALAMA NA WANAENDELEA VEMA. IKIWEZEKANA TOA MSAADA WA UNASIHI

### Muktadha

Ugonjwa wa COVID-19 umekuwa na athari mbaya kwa wafanyakazi wengi ikiwa ni pamoja na walimu duniani kote. Wafanyakazi wameathiriwa kiakili, kihisia na hata kiuchumi. Shughuli za shule zimeathiriwa, walimu walikuwa wanafanyia kazi nyumbani kwa kutumia njia za masafa katika ufundishaji , ambazo walikuwa hawazifanyii kazi hapo kabla, baadhi ya wafanyakazi mishahara yao imepunguzwa au mikataba imesimamishwa.  Baadhi ya wafanyakazi wamewapoteza wanafamilia, ndugu na marafiki zao kutokana na ugonjwa wa korona. Ni muhimu kuzingatia kwamba madhara ya ugonjwa huu yataendelea kuwepo wakati shule zinapofunguliwa.

Kwa hiyo, viongozi wa shule wanapaswa kuchukua hatua kuhakikisha afya na ustawi wa wafanyakazi wao wakati wanapitia katika kipindi hiki chenye changamoto.

## Utekelezaji katika Shule Yako

Wazo lifuatalo linaweza kuwasaidia viongozi wa shule kuzuia matumzi na kuhakikisha wafanyakazi kujiona wanasaidiwa wakati wa kipindi hiki cha korona. Hili linaweza kusaidia kuhamasisha ushirikishwaji wa wafanyakazi, imani na usalama, vitu ambavyo ni muhimu sana kwa kuzingatia mgogoro unaoendelea wa nguvukazi:

Wasiliana na wafanyakazi mara kwa mara wakati wa kipindi hiki, ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na mfanyakazi mmojammoja: Ni muhimu kwa waajiri kupanga angalau mpango wa wiki wa kuwafikia wafanyakazi wa shule. Tumia muda, sikiliza kwa makini na changia uzoefu na hisia na kila mfanyakazi. Hili linaweza kufanywa kwa kupiga simu, kutumia ujumbe mfupi wa maandishi, WhatsApp na njia nyingine zozote za mawasiliano zilizopo.  Viongozi wa shule pia wanaweza kukutana na wafanyakazi ana kwa ana iwapo hili linaruhusiwa katika nchi yako lakini kumbuka kufuata hatua kwa ajili yako na kwa ulinzi na usalama wa wafanyakazi wako.

Tafuta njia ndogo kuonyesha msaada na uangalizi wako kwa wafanyakazi kwa kutumia mbinu mbalimbali za ushirikishwaji: Inawezekana shule inapitia hali mbaya ya kifedha lakini jaribu kuwasaidia wafanyakazi kubainisha masuluhisho ya matatizo na kutafuta huduma za msaada pale ambapo inawezekana. Shirikianeni katika kusaidiana, na kuondoleana misongo, ukubwa wa kazi, na usalama wa kila mmoja.

- Kumbuka kuwauliza wafanyakazi wa shule jinsi wanavyoendelea na kujisikia, na jinsi familia zao zinavyoendelea, hakikisha kuwa wanasikilizwa na kueleweka.
- Jitolee kuwasaidia wafanyakazi kwa mahitaji ya msingi kama vile usafirishaji, muda wa maongezi na vifurushi vya intaneti iwapo hili linawezekana.
- Iwapo ikitokea kwamba shule inasitisha mikataba na walimu, inapunguza mishahara au kushindwa kuwalipa, inashauriwa kwamba suala hili lielezwe kwao kwa sababu za wazi wakati wa kukutana nao mmoja mmoja.
- Epuka kufanya uamuzi wa haraka bila ya kuwasiliana na wafanyakazi hususani kwa jambo linalowahusu..
- Wakati shule zinapofunguliwa tena, inawezekana kwamba bado zitaendelea kukabiliana na hali ngumu ya uchumi hata hivyo, shule zinapaswa kuhakikisha kwamba walimu wanaendelea kulipwa kwa wakati, hasa kwa kuwazingatia wenye mikataba isiyotabirika. Hili litawasaidia walimu kuendelea kubaki na kuimarisha ustawi wao.
- Tafuta njia za kuwatia moyo wale ambao wanafanya vizuri na hamasisha ushirikiano miongoni mwa wafanyakazi wako. Tambua hali ngumu na thamini mafanikio, hata kama ni madogo.

Hakikisha wafanyakazi wanachukua tahadhari binafsi: Wakumbushe wafanyakazi kufuata hatua zote za usalama kama inavyoshauriwa na Shirika la Afya Duniani na Wizara ya Afya katika nchi yako. Waulize wafanyakazi kuhusu mtandao wao wa kusaidiana na jinsi wanavyoupata wakati wa kipindi cha kujitenga kijamii. Wahamasishe kufanya mazoezi ya viungo. Hili litawasaidia kubaki salama na kupunguza misongo yao. Tahadhari ileile bado itakuwa muhimu wakati shule zitakapofunguliwa tena ili kuhakikisha wafanyakazi na wanafunzi wanalindwa.

Toa huduma ya unasihi kwa wafanyakazi ili wakabiliane na msongo, wasiwasi au hofu: Wakati vitu vingi vinapokuwa katika mashaka au juu ya udhibiti wetu moja ya njia bora zaidi ambayo tunaweza kudhibiti misongo na wasiwasi ni kuendelea kuyafanya yale ambayo yako chini ya udhibiti wetu. Zifuatazo ni baadhi ya njia unazoweza kuwashauri wafanyakazi wako kuchukua hatua za dhati kulinda ustawi wao wa kimwili na kihisia wakati wa kipindi hiki kigumu:

- Jifunze jinsi ya kujilinda na kuwalinda wengine dhidi ya COVID-19
- Thamini hisia zako
- Endelea na shughuli na taratibu zako zilezile za kila siku kadri iwezekanavyo

- Endelea kuwasiliana na familia na marafiki zako, kumbuka kuwa kuepuka msongamano haimaanishi kutowasiliana kabisa.
- Tafuta taarifa sahihi
- Weka ukomo wa habari na mitandao ya kijamii

## PANGA UWEZEKANO WA KUPUNGUZA WAFANYAKAZI KUTOKANA NA WALIMU KUTORUDI KWA SABABU ZA KIAFYA AU KIFEDHA. PANGA KUPITIA UPYA RATIBA ZA WAFANYAKAZI NA AJIRI WAFANYAKAZI WAPYA.

### Muktadha

Kutokana na shule kuendelea kufungwa kwa zaidi ya miezi miwili, viongozi wa shule wameathiriwa kifedha kiasi cha kutoweza kulipa mishahara ya walimu katika matukio mengi, wakiwaacha walimu watafute njia zingine za kuishi. Hili linaweza kusababisha baadhi ya walimu kutorudi baada ya shule kufunguliwa tena, hivyo kuwalazimu viongozi wa shule kuajiri walimu wapya. Katika baadhi ya matukio, walimu watasimamishwa pale ambapo shule haitaweza kulipa kutokana na matatizo ya kifedha. Katika matukio haya yote mawili, lazima kuwe na mpango mzuri wa utekelezaji.

Viongozi wa shule wawasaidie walimu kuendana na utaratibu mpya wakati watakapoanza tena kufundisha darasani. Walimu na wafanyakazi mwega wanahitaji kupewa msaada na rasilimali za kutosha kurudi katika maisha ya darasani, na kwa namna nyingine kutoa mafunzo ya msasa. Msaada huo ni wa muhimu hasa mkazo zaidi unaweza kuwekwa katika muda wa mwalimu.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Panga kwa ajili ya uwezekano wa wafanyakazi waliopungua kutokana na walimu kutorudi kwa sababu za kiafya au kifedha. Upangaji unaweza kujumuisha kupitia upya ratiba na kuajiri wafanyakazi wapya.

- Bainisha walimu ambao watarudu kazini baada ya shule kufunguliwa tena.
- Jiandae kuajiri wafanyakazi wapya iwapo kuna misuguano ya walimu. Hii inaweza kujumuisha:
    - Kwenda kwa mawakala wa magazeti ya ndani au mitandao ya shule ili kutangaza nafasi zilizo wazi.
    - Kupanga kuendesha usaili halisi kunapokuwa na zuio la kutotembea kutokana na zuio la kutotoka nyumbani.
- Panga vipindi zaidi kwa walimu ambao wamebaki shuleni. Kiongozi wa shule anaweza kutoa msaada zaidi, ikiwa ni pamoja na msaada wa kifedha katika matukio kama haya.
- Hakikisha kwamba sauti za walimu zinasikilizwa katika sera na mipango ili walimu waliobaki wahamasishwe na kuelewa sababu zinazotokana na mabadiliko ya kazi zao kuwa nyingi.
- Hamasisha mawasiliano ya wakati wote kwa wadau wote ili watambue masuala ambayo yanaweza kuathiri mahudhurio.
- Tafuta vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya shule ili uweze kuwalipa walimu.
- Fanya majadiliano na walimu yakilenga kurudi kazini.
- Rekebisha ratiba na mtaala wa darasa kulingana na mabadiliko ya muda wa shule, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa wanafunzi kwenda shuleni katika siku tofauti kutokana na kuepuka msongamano.
- Andaa vitini vya kufanyia kazi ambazo zinaweza kutumwa kwa wanafunzi wasiohudhuria shuleni kutokana na sababu za kiafya.

# WAKATI WA KUFUNGUA TENA.

## PITIA UPYA SERA ZA MAHUDHURIO YA WAFANYAKAZI ILI ZIJUMUISHE KUTOHUDHURIA KWA SABABU ZA KIAFYA.

### Muktadha

Wakati shule zinapofunguliwa tena, baadhi ya wafanyakazi wanaweza wakataka kuchelewa kujiunga kwa sababu za kiafya. Hizi zinajumuisha wafanyakazi au ndugu wa wafanyakazi wanaoonyesha dalili zinazohusiana na COVID-19. Katika matukio haya, kwa sababu ya ongezeko la hatua za kuzuia zilizochukuliwa na shule, kiongozi wa shule anaweza kumwomba mfanyakazi kusubiri. Kiongozi wa shule atahitajika kupitia upya sera za mahudhurio ili zijumuishe kutofika huko kunakotokana na sababu za kiafya.

### Utekelezaji katika Shule Yako

Katika mchakato wa kufundisha na kujifunza shuleni, fuata Taratibu Maalumu za Uendeshaji kama zilivyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) (kama vile Fikra za WHO kwa ajili ya hatua za kiafya za umma zinazohusiana na shule).

Kunaweza kukawa mabadiliko ya uendeshaji wa programu za kila siku za shule ikiwa ni pamoja na:

- Wafanyakazi kuhamasishwa kuwasiliana kwa haraka iwapo kuna tukio la ugonjwa wowote. Hili linaweza kufanywa kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi, kupiga simu au njia nyingine kwa viongozi wa shule.
- Kufanya marekebisho yanayofaa katika mipangilio au marekebisho ya ajira kwa wafanyakazi wanaotoka mbali.
- Kuwapatia majukumu mengine wafanyakazi wanaofanyia kazi nyumbani: Wafanyakazi wanaofanyia kazi nyumbani wanaweza kuwasaidia walimu kuandaa masomo ikiwa ni pamoja na kuandaa vitini vya kazi, ratiba na kuwasaidia viongozi wa shule katika kazi za uongozi, pale inapowezekana.
- Wafundishe walimu kuhusu njia halisi za kufundishia: Hili linaweza kusaidia iwapo walimu watatakiwa kujiweka karantini. Iwapo kuna ujifunzaji wa masafa, walimu hawa bado wanaweza kuwasaidia wanafunzi ambao hawaji shuleni kutokana na COVID-19
- Kutoa msaada wa kisiri na kitaalamu na huduma za ushauri ili kuwasaidia walimu ambao wanapitia magumu au kuhitaji taarifa za aina za huduma zilizopo.
- Kuwapeleka wafanyakazi kwenye vyanzo vya ushauri wa kitaalamu ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu Vituo vya Matibabu Vlivyothibitishwa vilivyopo katia eneo husika.

# ORODHAHAKIKI YA MPANGO WA KUFUNGUA TENA SHULE.

| USHIRIKISHWAJI WA WAFANYAKAZI | | | |
|---|---|---|---|
| KABLA YA KUFUNGUA TENA | | WAKATI WA KUFUNGUA TENA | |
| Wasiliana na wafanyakazi kila siku kuhakikisha kama wako salama na wanaendelea vema: Ikiwezekana toa msaada wa unasihi. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | Hakikisha malipo ya mishahara ya walimu yanaendelea na kufanyika kwa wakati, hususani kwa wale wenye mikataba isiyotabirika, ili kusaidia ubakiaji na ustawi wa mwalimu. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI |
| Hakikisha unafanya mawasiliano kwa wakati na walimu kuhusu mabadiliko katika utaratibu wa malipo. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | Hakiki sera za mahudhurio kwa wafanyakazi ili kujumuisha kutohudhuria kutokana na sababu za kiafya. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI |
| Panga kwa ajili ya uwezekano wa kupunguza wafanyakazi kutokanana walimu kutorudi kwa sababu za kiafya au kifedha; panga kupitia upya ratiba ya wafanyakazi na ajiri wafanyakazi wapya. | MHUSIKA<br><br>ITAFANYIKA LINI | | |